



Taarifa ya Mwenyekiti wa Bodi

Kasi Endelevu

Ninayo furaha kutangaza matokeo ya utendessji wa Kampuni ya Bia ya Tanzania Breweries Public Limited na kampuni zake tanzu, au TBL Group, kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Desemba 2023.

Imani ya soko katika kwenye vinywaji tunavozalisha na mkakati wa utangazaji vinadhihirishwa katika matokeo yetu. Licha ya changamoto za uendeshaji zilizojitokeza mwaka wa 2023, tuliweza kuendeleza ukuaji wa mapato pamoja na thamani ya muda mrefu kwa wanahisa wetu. Mwaka wa 2023 ulipata mchanganyiko wa changamoto zilizotokana na na athari za vita vya Urusi dhidi ya Ukraine na Israeli dhidi ya Hamas, wakati dunia ilikuwa bado ikipambana na athari sa janga la kimataifa la Uviko. Hivi vilichangia kuvuruga minyororo ya usambazaji wa kimataifa na ukwasi wa dola ya Kimarikani na hivyo kusababisha ongezeko kubwa la gharama za uzalishaji na uendeshaji. Ndani ya nchi, ongezeko kubwa la ushuru wa bidhaa kwenye malighafi zinazotumika katika uzalishaji wa bia, hali ya hewa ya mvua nyingi na mafuriko na mgawo wa umeme wa Tanesco, vilileta athari mbaya kwenye mauzo ya bia na kupunguza kasi ya ukuaji.

Pamoja na changamoto hizi, umaarufu wa (chapa za) bia na pombe kali zetu, na utekelezaji wetu bora wa mpango mkakati, vilichangia kuwezesha mwaka mwingine wa utendaji bora. TBL Group ilifanikiwa kupata ongezeko la mauzo na faida katika mwaka wa fedha 2023. Hali hii imewezesha Bodi ya Wakurugenzi kuidhinisha na kulipa gawio la TZS 537 kwa kila hisa (sawa na TZS 158,445 milioni) kwa mwaka 2023, ikiwa ni ongezeko la asilimia 85 dhidi mwaka uliotangulia. Hii inazingatia umuhimu wa kuongeza gawio kwa wanahisa kadiri hali ya kifedha inavyoruhusu.

Kuendelea na uwajibikaji kwa jamii

Tunajivunia kuwa miongoni mwa walipakodi wakubwa Tanzania. TBL Group ililipa TZS 586 bilioni za kodi mwaka 2023 ikilinganishwa na TZS 528 bilioni mwaka uliotangulia. Vile vile, TBL Group inaendelea kuongeza uwekezaji nchini, ikiwemo katika kilimo. Mnamo Julai 2023, Kampuni ilitangaza uamuzi wake wa kuwekeza na kuboresha kiwanda cha Kilimanjaro Malting (kiwanda cha kuchakata kimea). Mpango wa muda wa kati ni kusindika hadi tani 28,000 za shayiri kutokana na jumuiya za wakulima wa Tanzania, ili zitumike katika kutengenezea bia

zetu. Tumejitolea kuwawezesha wakulima kupitia mbinu za kisasa za kilimo, ujuzi wa biashara na fedha, ambavyo vitaongeza mnyororo wa thamani na kuwanufaisha wakulima wa shayiri, mtama na zabibu. Kwa sasa, TBL inanunua zaidi ya asilimia 74 ya malighafi yake kutoka nchini. Aidha, TBL Group inatoa nafasi za kazi zaidi ya milioni moja, moja kwa moja na kwa njia isiyo ya moja kwa moja, katika mzunguko wetu wa ugavi. Kwa miaka mingi, mafanikio haya yameimarisha nafasi yetu kama mwajiri na mzalishaji mkuu Tanzania

Kuhakikisha wakati ujao wenye furaha tele

Tukitarajia mwaka wa 2024, tunaamini kuwa tasnia rasmi ya vinywaji vya pombe inaendelea kuwa muhimu nchini Tanzania na kuna fursa zaidi mbele ya kupanua masoko yetu ya bia na vinyaji vingine. Tutaendelea kuwaweka wateja wetu mbele katika ya kila tunachofanya na kuendelea kutekeleza mpango wetu wa kibiashara uliojaribiwa ili kuharakisha kasi ya ukuaji wa biashara. Tumedhamiroa kuwa na ukuaji endelevu, wenye faida kwa kuendelea kuwekeza katika chapa zetu, vifaa vya uzalishaji na mabadiliko ya kidijitali.

Kwa kumalizia, ningependa kutoa shukrani za Bodi kwa wateja wetu wengi waaminifu na washirika wa kibiashara. Wamekuwa muhimu katika ukuaji wa biashara zetu unaoendelea na madhumuni yetu ya kuwezesha wakati ujao ambapo sote tunaweza kukusanyika na kusherehekea. Zaidi ya hayo ninatoa shukurani zangu za dhati wafanyakazi na wasimamizi wao wote kwa kujitolea kwao bila kuyumba katika kuendeleza TBL Group. Pia ningependa kutoa shukrani zangu kwa kila mmoja wa wanahisa wetu kwa kutuunga mkono na kwa Bodi yetu kwa kuzingatia viwango vya juu zaidi vya usimamizi.

Mwisho, ningependa kushukuru kwa kazi muhimu ambayo serikali yetu inatekeleza katika kuweka mazingira mazuri ya biashara na tunaahidi kuendelea kufanya kazi pamoja na kujitahidi kuongeza ubora siku zote.

Mwenyekiti wa Bodi

Leonard Mususa